JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI

**TUME YA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI**

***Ukijibu tafadhali taja:"***

**Kumb. Na**. CA.474/505/01/78 **Tarehe**: 16 Mei, 2025

Wakuu wa Taasisi za Umma na
za Binafsi (Public Private Sector)
**TANZANIA BARA.**

**Kuh: Mwaliko wa Mafunzo ya kupunguza Madhara ya Vihatarishi katika Ulinzi wa Taarifa Binafsi (Mitigating Data Risks: Integrating Risk Management with Personal Data Protection Compliance)**

Tafadhali rejeeni somo tajwa hapo juu.

2. Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) iliyoanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi Sura ya 44, kwa kushirikiana na Taasisi ya Usimamizi wa Vihatarishi Tanzania (IRMT) kwa pamoja tumeandaa mafunzo kwa Wakurugenzi, Mameneja, Wakuu wa Vitengo mbalimbali na Watumishi wengine wanaochakata taarifa (data) yatakayoendeshwa kuanzia **tarehe 23 - 25 Juni, 2025** katika Hoteli ya LUSH GARDEN iliyoko SAKINA Mkoani Arusha.

3. Mafunzo hayo ni muhimu kwasababu yamelenga kuwajengea uwezo washiriki kuhusu namna ya kupunguza madhara ya vihatarishi (risks) katika ulinzi wa taarifa za watu binafsi katika Taasisi, na pia kutekeleza miongozo inayotolewa na PDPC.

4. Kutokana na umuhimu wa mafunzo hayo, PDPC inakuomba uwaruhusu na kuwawezesha watumishi hao wahudhurie mafunzo hayo ili kuongeza ujuzi na kubadilishana uzoefu.

5. Ada ya mafunzo hayo ni **Tzs. 750,000** kwa mshiriki kwa ajili ya kukidhi gharama za ukumbi, shajala, mafunzo na chakula wakati wa mafunzo. Kwa maelezo kuhusu namna ya kujisajili na kufanya malipo unaombwa kuwasiliana na Bw. Rajabu Kabeya kupitia namba ya simu +255(0)715680150 au barua pepe rajabu.kabeya@pdpc.go.tz.

6. Ninashukuru kwa ushirikiano wenu.

Dkt. Emmanuel L. Mkilia(PhD)
**MKURUGENZI MKUU**

**Nakala:** Mtendaji Mkuu,
Taasisi ya Usimamizi wa Vihatarishi Tanzania (IRMT),
Ubungo Plaza Ghorofa la Pili,
S.L.P 71902,
**DAR ES SALAAM.**